VIJANA NA VYAMA VYA WAFANYAKAZI

Chama cha wafanyakazi ni nini?

Chama cha Wafanyakazi ni muungano wa wafanyakazi ulioanzishwa na wafanyakazi wenyewe kwa madhumini ya kudai, kulinda na kutetea haki na maslahi yao.

Madhumuni ya Chama

- Kuboresha kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini
- Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kuunda kamati za majadiliano na kuanzishwa kwa Mabaraza ya wafanyakazi ili kudumisha amani mahali pa kazi
- Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya Mwajiri na Mwanachama
- Kujadil,i kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Hali bora ya kazi.
- Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na Vyama vingine vya wafanyayakazi nchini pamoja na vile vya kimataifa
- Kuwasiliana na serikali kuhusu haja ya kutunga sheria sahihi za kazi na sera nzuri za kuendeleza uchumi na maisha ya jamii
- Kulinda maslahi ya wanachama kwa kuisaidia serikali ili kuepukana na uandaaji wa sera ambazo hazina manufaa kwa wafanyakazi

Kijana ni nani?

Kijana ni mtu yeyote mume au mke aliye kati ya umri wa miaka 18 mpaka 35.

Je kuna Changamoto gani inaweza kukukabili wewe kijana wa Chama cha wafanyakazi/

- Inawezekana wakati wa kudai haki yako ukaachishwa kazi au kufukuzwa kazi hususani unapofanya kazi na mwajiri mkorofi
- Inawezekana ukashindwa kutekeleza majukumu yako wewe kama kijana kiongozi wa Chama cha wafanyakazi ama kwa kukosa ushirikiano na mwajiri wako au viongozi wenzako
- Inawezekana ukashindwa kuhamasisha vijana wenzako kujiunga na Chama
- Inawezekana ukashindwa kutetea haki na maslahi ya vijana wafanyakazi wenzako hususani wakati wa kudai maslahi yenu

Kwa nini kijana ujiunge na Vyama vya wafanyakazi?

- Ili ujue haki na maslahi yako

- Ili upate utetezi wakati wa kushughulikia migogoro au katika kushughulikia malalamiko yako
- Ili upate usalama wa ajira yako
- Ili upate elimu zitolewazo na Vyama vya wafanyakazi
  hususani masuala ya elimu ya sheria za kazi, Afya na usalama mahali pa kazi, na Ukimwi
- Ili upate fursa na nafasi ya kushiriki katika majadiliano na mwajiri wako katika kukabiliana na masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na tija na kuboresha mazingira ya kazi yako
- Ili ujenge mahusiano mazuri na bora baina ya kijana mfanyakazi na mwajir wako ambayo huleta maisha bora kwa upande wako na ongezeko la uchumi kwa upande wa mwajiri
- Ili ujenge mahusiano/ushirikiano na vijana wenzako kutoka sekta/zingine nchini au hata nje ya nchi.
- Ili ubadilishane uzoefu na kijana/vijana wenzako wa sekta zingine.

Sisi kama vijana wanachama wa TUICO ni namna gani tutahamasishana wafanyakazi vijana kujiunga na Chama?

- Hatuna budi kushauri Chama kufanya mabadiliko ya namna ya uendeshaji wa shughuli zake ili kuwavutia vijana wengine kushawishika kujiunga. Hii ni pamoja na kwenda na wakati ili kukabiliana na changamoto zinazowakumba vijana. Teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na matumizi bora ya mitandao ya mawasiliano kuwafikia wafanyakazi vijana.

- Chama kuandaa mpango tathmini wa matatizo yanayowakumba vijana katika soko la ajira pamoja na kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za Chama.

- Vijana tuhamasishe chama kuwawezesha vijana kuingia katika soko la ajira, hii ni pamoja na kipitia sera ya taifa ya ajira ili iweze kuweka mazingira mazuri ya vijana kupata kazi mara wanapohitimu masomo yao

- Tunatakiwa kusisitiza kuwajengea uwezo vijana juu ya ufahamu wa masuala yanayohusu Chama mfano Katiba na Muundo wa TUICO, Sheria za Kazi, Misingi na majukumu ya Chama cha Wafanyakazi, Haki na Wajibu wa mwanachama

- Kushiriki katika kampeni mahususi kwa ajili ya kuwahamasisha vijana ili kujiunga na Chama cha wafanyakazi.. Chama pamoja na mambo mengine ni lazima kielezee mafanikio yake mara kwa mara kwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari

- Chama cha wafanyakazi ni sharti kiwe na muundo wa vijana ambao unawawezesha vijana kushiriki moja kwa moja katika ngazi zote za maamuzi na uongozi kwa ujumla. Kwa hiyo basi Kamati za Vijana zianzishwe kuanzia ngazi ya Tawi hadi Taifa

- Chama lazma kiwe na Idara ya Uhamasishaji ambayo itaratibu shughuli za uhamasishaji kwa ujumla ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa Wafanyakazi vijana.

- Vijana wahamasishwe ili waweze kugombea katika nafasi mbalimbali za uongozi

- Chama kiweke mazingira ya vijana kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, ziara za mafunzo na hata kuwa na mikutano na vijana wa sehemu nyingine za kazi ili wabadilishane uzoefu.

Je unawezaje kujiunga na TUICO?

- Nenda Ofisi ya TUICO iliyoko Mkoani kwako uonane na ofisa wa TUICO ili aweze kukuandikisha kuwa mwanachama kwa kujaza Fomu namba 6 kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.
- Mtendaji wa Chama atakupatia kadi ya TUICO pamoja na maelezo ya ujumla kuhusu suala zima la uanachama na faida za kuwa mwanachama na ushiriki wako katika Chama ili uwe mwanachama hai daima
- Tembelea Tovuti ya TUICO (www.tuico.or.tz). Yapo maelezo na fomu ya kujiunga na chama.